This is a digital copy of a book that was preserved for generations on library shelves before it was carefully scanned by Google as part of a project to make the world's books discoverable online.

It has survived long enough for the copyright to expire and the book to enter the public domain. A public domain book is one that was never subject to copyright or whose legal copyright term has expired. Whether a book is in the public domain may vary country to country. Public domain books are our gateways to the past, representing a wealth of history, culture and knowledge that's often difficult to discover.

Marks, notations and other marginalia present in the original volume will appear in this file - a reminder of this book's long journey from the publisher to a library and finally to you.

Usage guidelines

Google is proud to partner with libraries to digitize public domain materials and make them widely accessible. Public domain books belong to the public and we are merely their custodians. Nevertheless, this work is expensive, so in order to keep providing this resource, we have taken steps to prevent abuse by commercial parties, including placing technical restrictions on automated querying.

We also ask that you:

+ *Make non-commercial use of the files* We designed Google Book Search for use by individuals, and we request that you use these files for personal, non-commercial purposes.

+ *Refrain from automated querying* Do not send automated queries of any sort to Google's system: If you are conducting research on machine translation, optical character recognition or other areas where access to a large amount of text is helpful, please contact us. We encourage the use of public domain materials for these purposes and may be able to help.

+ *Maintain attribution* The Google "watermark" you see on each file is essential for informing people about this project and helping them find additional materials through Google Book Search. Please do not remove it.

+ *Keep it legal* Whatever your use, remember that you are responsible for ensuring that what you are doing is legal. Do not assume that just because we believe a book is in the public domain for users in the United States, that the work is also in the public domain for users in other countries. Whether a book is still in copyright varies from country to country, and we can't offer guidance on whether any specific use of any specific book is allowed. Please do not assume that a book's appearance in Google Book Search means it can be used in any manner anywhere in the world. Copyright infringement liability can be quite severe.

About Google Book Search

Google's mission is to organize the world's information and to make it universally accessible and useful. Google Book Search helps readers discover the world's books while helping authors and publishers reach new audiences. You can search through the full text of this book on the web at `http://books.google.com/`



KATEKISIMO FUPI.

MAFUNDISHO

KWA

MAULIZO NA MAJIBU.

SO
LI
DEO
GL
OR
IA



ZANZIBAR.
1876.

141. n. 93.

PRINTED AT THE UNIVERSITIES' MISSION PRESS, ZANZIBAR.

I.

Nani aliyekuumba?
Muungu.
Yuko wapi Muungu?
Mahali pote, mbingu na inchi zimejaa naye.
Muungu ni nini?
Ni Roho.
Muungu alikuwa na mwanzo?
Siyo kabisa.
Ni miungu mingapi?
Muungu ni mmoja tu.
Katika Muungu inayo nafsi moja tu?
Zinazo nafsi tatu.
Nafsi hizo, ndizo zipi?
Muungu Baba, Muungu Mwana, na Muungu Roho Mtakatifu.

Muungu Mwana na Muungu Roho Mtakatifu walikuwa na mwanzo ?

Siyo, walikuwa tangu milele pamoja na Muungu Baba.

Ni hawa miungu mitatu?

Siyo, nafsi tatu, lakini Muungu mmoja kabisa.

Muungu aona na ajua vitu vyote ?

Ndio, ajua mawazo yetu yote pia.

Yee aweza kufanya vitu vyote ?

Ndio, ni 'Mweza killa kitu.

Yee ameviumba vitu vyote ?

Ndio, ameviumba pasipo kwanza kitu.

Katika majira gani ameviumba?

Katika siku sita.

Kwa nani ameviumba ?

Kwa neno lake.

Neno lake ni nani ?

Muungu Mwana.

II.

Nani aliyekukomboa?

Isa Masiya, ndiye Muungu Mwana aliyefanywa mwana adamu kwa sababu yetu.

Amekukomboaje?

Ameninunua kwa kufa kwake.

Amekukomboa katika aini ?

Katika nguvu ya Shetani.

Isa Masiya ndiye Muungu ?

Ndio, ni Muungu hálisi ya Muungu hálisi.

Isa Masiya ndiye mwana adamu ?

Ndio, ni tena kwa kweli mwana adamu.

Katika Isa Masiya sinazo nafsi ngapi ?

Moja, ndiye Muungu Mwana.

Ni asili ngapi katika Isa Masiya ?

Mbili, asili ya Muungu, na asili ya mwana adamu.

Kwa ajili gani Muungu Mwana amefanywa mwana adamu ?

Atutoe sisi katika thambi na jehannum.

III.

Alikuwa Bwana wetu Isa Masiya sikuzote mwana adamu ?

Siyo.

Tangu lini ni mwana adamu ?

Zayidi ya miaka themantashara mia.

Amekuwaje mwana adamu ?

Alizaliwa na Maryamu mwanamwali aliobarikiwa.

Kwa nguvu gani ?

Alichukuliwa mimba kwa Roho Mtakatifu.

Amekwisha kuwa Muungu ?

Siyo, ni Muungu pamoja na mwana adamu.

Atakuwa hivyo siku zote ?

Ndiyo, hatta milele.

Katika mambo gani amezaliwa Bwana wetu Isa Masiya ?

Katika mambo masikini.

Kwaje ?

Amezaliwa katika banda mjini Betlehemu.

Hali gani aliyoipata duniani ?

Hali ya taabu na huzuni.

Kwa sababu gani ?

Amechukiwa na Shetani na watu wenyi thambi.

Kwa ajili gani amesumbuka vibaya ?

Kwa sababu ya thambi zetu.

IV.

Alisumbukaje Bwana wetu Isa Masiya ?

Kwa kitisho katika bustani na hari ya damu.

Kwa nini tena ?

Walimfanyizia mzaha, wakamtukana.

Kwa nini tena ?

Alipigwa, akavikwa taji ya miiba, akachukua msalaba wake.

Kwa nini tena ?

Alifungwa msalabani kwa mismari hatta akafa katikati ya wanyang'anyi wawili.

Kwa siku ipi alipokufa ?

Juma.

Aliuawa wapi ?

Kalvarini, mbele ya mlango wa 'mji Yerusalemi.

Kwa ajili gani alikufa ?

Kuirithika haki ya Muungu na kuzisetiri thambi zetu.

V.

Alipokwisha kufa Bwana wetu Isa Masiya alikuwaje ?

Mwili wake ulizikwa, roho yake ikashuka mahali pa wafu.

Mwili wake ukaharibika ?

Haukuharibika.

Alifanyani tena ?

Aliondoka katika kaburi.

Kwa siku ipi ?

Juma a pili.

Alifanyani tena ?

Akapaa mbinguni.

Alipopaa lini ?

Siku arobaini baada ya kufufuka.

Akapaa kwa siku ipi?

Alhamisi.

Yuko wapi sasa?

Anakaa mkono wa kuume wa Muungu.

Muungu hana mkono, mkono wake wa kuume nini?

Ndio kwa mfano mahali pa heshima kuliko yote.

VI.

Atakaa sikuzote mkono wa kuume wa Muungu?

Siyo, atarudi.

Atarudi lini?

Kwa siku ya mwisho.

Atakaporudi atafanyani?

Atawaamua walimwengu.

Atatuamuaje?

Kwa vitendo tulivyovifanya katika mwili.

Atatuamua kwa vitendo tu?

Kwa vitendo vyetu, maneno yetu na mawazo yetu yote pia.

Atakujaje?

Kwa nguvu na utukufu mkuu.

Atawaambiani watu wabaya ?

Enendeni enyi 'mmelaaniwa, motoni mwa milele.

Atawaambiani watu wema ?

Njooni, enyi waliobarikiwa na Baba yangu.

Nani watakaotupeleka barazani kwa hukumu ?

Malaika watakatifu.

VII.

Itakapokwisha hukumu, wabaya watapatani ?

Watatupwa motoni mwa jehannum, na mwili na roho pamoja.

Watasumbukaje ?

Watachomewa na wataumizwa milele.

Wenzi wao nani ?

Shetani na malaika zake.

Shetani nani ?

Pepo aliyeanguka mbinguni kwa sababu ya kiburi chake.

Hukumu itakapokwisha, watu wema watapatani ?

Wataingia mbinguni pamoja na Masiya.

Mbinguni watapatani ?

Watafurahiwa milele na Mungu.

VIII.

Nani anayekutakasa ?

Muungu Roho Mtakatifu.

Anakutakasaje ?

Akinifanya mtu mwema na mtakatifu.

Akufanyaje mwema ?

Kwa kukaa nami.

Ametoka wapi huyo Roho Mtakatifu ?

Ametoka katika Baba na Mwana.

Yee ni sawa na hawa ?

Ndio, yee pamoja nao Muungu mmoja na Bwana mmoja.

Amekuja tangu lini kukaa naswi duniani ?

Juma ya pili ya Pentekoti.

Anakaa na watu gani ?

Anakaa katika Kanisa lo takatifu na lo katoliko.

IX.

Kanisa lo takatifu nini ?

Mwili wa Masiya.

Mwili huu nini ?

Watu wote wanaoamini wanaambatana kwa kuwa na kitwa kimoja.

Kitwa hiki nani ?

Masiya Isa Bwana wetu.

***Niambie* sifa za Kanisa la Masiya.**

Ni moja, ni takatifu, ni Katoliko, ni Apostoliko.

Katoliko — maana yake nini ?

Kwa wote, mahali pote, na lenyi kweli yote.

Apostoliko — maana yake nini ?

Liliowafuata kwanza Apostoli, ndio mitume wake Masiya, likafuata hatta leo askafu.

Usharika wa watakatifu nini ?

Watakatifu wote wanashariki neema ya Muungu na vitu vyema vyote.

Mtu gani ni mtakatifu ?

Mtu anayemtumikia kwa moyo Muungu, ao hapa katika inchi, ao huko katika mbingu.

Usharika nini ?

Watu wengi wenyi kitu kimoja.

Kanisa la Masiya linayo mafungu mangapi ?

Mawili, Kanisa liliokwisha kushinda na Kanisa lifanyalo vita.

Liko wapi Kanisa liliokwisha kushinda ?

Mbinguni.

Liko wapi Kanisa lifanyalo vita ?

Hapa, katika inchi.

Kanisa lifanyalo vita, linalo mafungu mangapi ?

Mawili, Padre, ao Wangoje, na watu.

Padre watu gani ?

Tame za Muungu.

Zinazo ginsi ngapi za Padre ?

Tatu, Asikafu, Kasisi, na Shemasi.

X.

Thambi ndio nini ?

Kuivunja sheria ya Muungu.

Zinazo ginsi ngapi za thambi ?

Mbili, thambi ya asili na thambi za amali.

Thambi ya asili nini ?

Ndiyo upungufu kwa asili, siswi wote tumezaliwa wenyi thambi hii.

Thambi za amali nini ?

Thambi zote tulizozifanya siswi wenyewe.

Thawabu za thambi nini?

Kufa na moto wa Jehannum.

Thambi zinaondokaje ?

Kwa sababu ya mateso na mauti ya Bwana wetu Isa Masiya.

Thambi zetu zinaondoshwa lini ?

Katika ubatizo.

Katika majira gani tena ?

Wakati wa kutubu.

Kutubu nini ?

Kuzichukia na kuziacha thambi zetu.

XI.

Siri ya dini yetu, ndio nini ?

Kitu kwa 'nje kinachoonyesha neema iliopo kwa ndani.

Siri ngapi zimewapasa watu wote ?

Mbili, siri ya Ubatizo, na siri ya Mwili na Damu ya Bwana.

Nana aliyeziamurn siri hizi ?

Bwana wetu Isa Masiya.

Ameziamuru wapi ?

Katika Kanisa.

Kwani ameziamuru ?

Zituletee neema.

Neema ndio nini ?

Msaada na upendeleo wa Muungu.

Siswi tunaweza kufanya neno jema pasipo neema ?

Siyo, hatuwezi.

Tupateje neema ?

Kwa kusali na kwa siri takatifu.

Kusali nini ?

Kuinua roho kwa Muungu.

Neema za siri zimetoka wapi ?

Zinatoka katika sadaka ya kufa kwake Bwana wetu Masiya.

XII.

Umebatizwa kwa kitu gani?

Kwa maji.

Umebatizwa kwa jina gani?

Kwa jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu.

Wakati wa kubatizwa umefanya nini?

Nimefanya maagano na Muungu.

Umefanya ahadi gani?

Kumchukia Shetani na kazi zake.

Kazi za Shetani nini?

Thambi zote na makosa yote.

Umefanya tena ahadi gani?

Kuiamini Imani masihiya.

Maana yake kuamini?

Kusadiki na kukubali.

Nione wapi walivyoviamini Wamasihiya?

Katika Imani zetu.

Umefanya tena ahadi gani?

Kuzishika amri zote za Muungu.

Muungu amekufanya nini?

Amenifanya kiungo cha Masiya.

Nini tena?

Mtoto wa Muungu.

Nini tena?

Mrithi ufalme wa mbinguni.

Neema halisi ya ubatizo nini ?

Neema ya kuzaliwa kwa roho, na kutakasika kabisa.

Kuzaliwa kwa roho, maana yake ?

Kupata uzima mpya na mtakatifu.

XII.

Siri ya pili nini ?

Siri ya Mwili na Damu ya Bwana.

Kwani ameiamuru Bwana wetu ?

Itukumbushe kufa kwake.

Kwa maksudi gani tena ?

Itulctee pato la kufa kwake.

Fungu kwa 'nje ya siri hii nini ?

Mkate na divai.

Fungu kwa ndani nini ?

Mwili na Damu yake Masiya.

Ni siri tu ?

Ni tena sadaka masihiya.

Sadaka maana yake nini ?

Kitu alichopewa Muungu.

Neema hálisi ya siri hii nini ?

Kupata chakula cha roho.

XIV.

Tutakapokwisha kufa tutakuwaje?

Miili yetu itakuwa vumbi.

Roho zetu zitakuwaje ?

Zitangoja mwisho wa ulimwengu.

Kwa siku ya mwisho zitafanyaje ?

Zitaungana na miili.

Kwani ?

Tuamuliwe katika roho na mwili pamoja.

Vitu vinne vya mwisho vipi ?

Kufa, Hukumu, Mbingu na Jehannum.

Imetupasa kuvifikiri vitu hivi ?

Ndio, imetupasa kuvifikiri sana.

Imetupasa kufikiri nini tena ?

Uzima na mauti ya Bwana wetu Isa Masiya.

Imetupasa kukumbuka sikuzote nini ?

Ya kwamba Mwenyiezi Muungu anatuona.

Tumtumikieje ?

Kwa Imani, kwa Matumaini, na kwa Mapenzi.

Vitendo vyetu pia vifanyweje ?

Kwa sifa na heshima ya Muungu.

Utukufu uwe kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu, ulivyokuwa mwanzo, ulivyo sasa, utakavyokuwa milele.

Amina.